

Idara ya Elimu ya NSW

# Kuingia Year 7 katika Shule ya Serikali ya NSW

## Fanya ombi mtandaoni ili kuanza mpito wa mtoto wako kutoka Year 6 hadi Year 7.

### Shule ya mtaani ya mtoto wako

Shule nyingi za Serikali za NSW zina maeneo yanayotengwa ya mwingilio ili watoto wote wenye umri wa kwenda shule watastahili kuhudhuria shule ya serikali – shule yao ya mtaani.

Anwani ya kudumu ya makazi ya mtoto wako huamua ni shule gani ni shule ya mtaani ya mtoto wako. Kifaa cha The School Finder (Kutafuta Shule) kwenye education.nsw.gov.au/school-finder kinaweza kukusaidia kuipata shule ya mtaani.

Wazazi na walezi wengi katika NSW huchagua shule zao za mtaani ili kutoa elimu bora kwa mtoto wao. Mfumo wa idara wa kujiandikisha mtandaoni husaidia mpito kwa shule ya juu.

Shule za mitaa huhudumia wanafunzi wa viwango vyote vya uwezo, ikijumuisha miradi ya kuwapa changamoto wanafunzi wenye uwezo na vipawa vya juu na miradi kwa wanafunzi walio na mahitaji ya ziada ya kujifunza na usaidizi. Pia hutoa shughuli mbalimbali za ziada za mitaala.

Kuna vyuo vya kampasi nyingi ambavyo vinajumuisha idadi ya shule au kampasi, na kila shule au kampasi kitaalam katika maeneo tofauti. Kwa mfano, kuna kampasi za wadogo (Years 7-9 au 7-10), kampasi za wakubwa (Years 10-12 au 11-12), kampasi zinazochagua kitaaluma, kampasi za mafunzo ya jinsia pamoja na kampasi za jinsia moja.

Kuna shule za kati pia ambazo zinatoa fursa kwa jamii nyingi za vijijini na zilizotengwa kuwasomesha watoto wao kutoka kwa Kindergarten hadi kwa Year 12 katika mazingira ya shule moja. Shule nyingi za kati hutumia teknolojia kuunganisha walimu na wanafunzi katika shule tofauti ili masomo mbalimbali hutolewa. Shule za kati pia zinatoa shughuli mbalimbali za ziada za mtaala.

Ikiwa huwezi kufanya ombi mtandaoni au hutapendelea, ujaze fomu kuanzia ukurasa wa 5 wa kijitabu hiki. Tuma fomu iliyojazwa kwa shule ya msingi ya mtoto wako.

Maelezo zaidi yanapatikana kwenye
education.nsw.gov.au/public-schools/going-to-a-public-school/enrolment/high-school-enrolment

# Chaguzi nyingine za shule

## Unaweza kuwa na sababu kwa nini ungependa mtoto wako ahudhurie shule ambayo sio shule ya mtaa wako.



## Shule ambazo zisizo za mtaa (au nje ya eneo)

Shule zilizo na eneo maalum la uandikishaji zina kikomo cha uandikishaji – idadi ya wanafunzi ambayo wanaweza kuandikishwa kulingana na makazi ya kudumu ya shule. Kikomo cha kujiandikisha kinatuambia kama shule inaweza au haiwezi kukubali uandikishaji usio wa mtaa. Katika kikomo cha kujiandikisha, baadhi ya shule zinaweka kiwango cha bafa ya uandikishaji wa mtaa ili kutenga nafasi kwa wanafunzi wa mtaa wanaofika wakati wa mwaka.

Shule ambazo zimefika au zinakaribia kikomo chao cha uandikishaji hazitaandikisha wanafunzi wasio wa eneo, isipokuwa kama kuna mazingira ya kipekee.

Hata hivyo, shule ambazo zina nafasi chini ya kiwango cha bafa zinaweza kukubali wanafunzi wasio wa mtaa.

Katika shule ambazo mahitaji ya uandikishaji usio wa mtaa yanazidi idadi ya nafasi yaliyopo chini ya bafa, shule lazima zitengeneze vigezo vya uandikishaji wa nje ya eneo na kanzisha jopo la uteuzi ili kuzingatia maombi yasio ya mtaa.

## Shule za kitaalamu

Shule za kitaalamu hutoa elimu ya sekondari ambayo inazingatia vipaji au maslahi maalum. Shule za kitaalamu zimeanzishwa kwa sanaa za ubunifu, za maonyesho na za kuona, lugha, teknolojia (ikiwa ni pamoja na teknolojia ya baharini na teknolojia ya vijijini), kilimo na michezo.

Katika baadhi ya shule hizi za kitaalamu vigezo vya uandikishaji vinaweza kujumuisha maonyesho au jaribio.

## Madarasa ya usaidizi

Baadhi ya shule za sekondari zina madarasa ya usaidizi ili kuhudumia mahitaji ya ziada ya kujifunza na ya msaada wa wanafunzi wenye ulemavu.  Mkuu wa shule ya msingi ya mtoto wako atakusaidia kupata chaguo sahihi la shule kwa mtoto wako, kwa kuzingatia chaguo lako, mahitaji maalum ya ziada ya kujifunza ya mtoto wako na ukaribu wa huduma za wataalamu wa mtaa.

Kuzingatia uwekaji katika darasa la usaidizi husimamiwa kupitia mchakato wa uwekaji.

## Shule zinazochaguliwa kitaaluma

Mchakato wa maombi ya kuingia katika shule iliyochaguliwa kikamilifu au kwa kiasi fulani kitaaluma huanza wakati mwanafunzi yupo Year 5 na ni mrefu kuliko mchakato wa kawaida wa uandikishaji.

Fomu ya maombi inapatikana tu mtandaoni. Tafadhali kumbuka kuwa hakuna maombi ya kuchelewa yatakayokubaliwa.

Orodha ya shule zilizochaguliwa  kitaaluma na maelezo ya taratibu zao za uandikishaji zinapatikana kwa: https://education.nsw.gov.au/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes

## Vituo vya Kiingereza cha Kina

Tumia Kifaa cha Kutafuta Shule kwenye: https://education.nsw.gov.au/school-finder kupata shule za pili zinazotoa msaada wa Kiingereza cha Kina.

Toa anwani yako ya nyumbani au msimbo wa posta ili kutafuta ramani ya shule yako ya mtaa na uchague kifute cha Intensive English Centre kwenye “Nearby schools”.

Ili kupata maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na mkuu wa shule ya msingi ya eneo lako au shule ya pili ya uchaguzi wako.

Iwapo unahitaji mkalimani ili kukusaidia na ulizo lako tafadhali pigia simu **Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye** 131 450 na omba kupata mkalimani katika lugha yako. Huduma hii itakuwa bila malipo kwako..

# Kukamilisha Usemi wa Nia

## Unaweza kuonyesha ungependa mtoto wako ahudhurie shule gani kwa kujaza fomu ya Usemi wa Nia kwa shule la mtaa wako na/au kiwango cha juu cha shule za nje ya eneo.

Kuna hatua tatu za kumwandikisha mtoto wako katika Year 7:

## Hatua ya 1: Jaza Usemi wa Nia ili kuomba uwekaji katika shule ya/za serikali ya/za uchaguzi wako.

### Fomu hii inapaswa kujazwa kwa Kiingereza na wazazi na walezi wa wanafunzi wote wanaoomba kuwekwa katika Year 7 katika shule ya serikali ya NSW mwaka ujao.

Kwa wanafunzi ambao wameandikishwa kwa sasa katika shule za msingi za Serikali ya NSW unaweza kujaza semi la nia mtandaoni au kujaza fomu ya karatasi inayoambatanishwa hapa na ituma kwa shule ya msingi ya mtoto wako. Kwa wanafunzi ambao hawajaandikishwa kwa sasa katika shule za msingi za Serikali ya NSW unaweza kujaza semi la nia mtandaoni au ituma fomu hii kwa shule ya sekondari ya Serikali ya NSW unayokusudi kumwandisha mtoto wako.

**Masemi yote ya Nia lazima yarudishwe kabla ya au kwa tarehe iliyowekwa.**

## Hatua ya 2: Kamilisha ombi la kujiandikisha

Mara baada ya mtoto wako kupewa nafasi katika shule, utaombwa kujaza **Ombi la kujiandikisha katika shule ya serikali ya NSW**. Hii itatumwa kwako wakati wa Kipindi cha 2 au Kipindi cha 3.

Ombi hili linaweza kukamilika mtandaoni au kwa kujaza fomu ya karatasi ambayo itatumwa kwako wakati wa Kipindi cha 2 au Kipindi cha 3.

Tafadhali kamilisha maelezo yote kwenye fomu hii na uirudishe haraka iwezekanavyo.

Uamuzi wa mwisho juu ya uandikishaji utafanywa kufuatia kuzingatia na kukubali ombi lako la kujiandikisha na mkuu wa shule. Mkuu anaweza kuwasiliana na wewe kwa habari zaidi.

Utapokea barua pepe au barua ya kuhakikisha kama mtoto wako amekubaliwa kuandikishwa au la.

## Hatua ya 3: Jua kuhusu shule yako mpya

Mara tu unapopokea uthibitisho wa uandikishaji wa mtoto wako, ni muhimu kujifunza kuhusu shule mpya ili kusaidia mtoto wako kuhamia kwa Year 7.

Shule itaandaa shughuli za mpito na siku ya mwelekeo kwa wanafunzi ambao wataanza Year 7 mwaka unaofuata. Wazazi na walezi kwa kawaida hualikwa katika siku hii ya mwelekeo, ambayo hufanyika mwishoni mwa Novemba au mapema mwa Desemba. Inamsaidia mtoto wako kujua kuhusu masomo katika shule za pili, walimu, madarasa na taratibu za shule, na hutoa fursa ya kukutana na wanafunzi wenzake.

Utashauriwa tarehe ya siku ya mwelekeo na shule yako mpya, pamoja na habari kuhusu sare, chaguzi za kusafiri na maelezo mengine muhimu.

Kama unahitaji maelezo zaidi tafadhali piga simu kwa mkuu wa shule. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye **131 450** na kuomba mkalimani. Mwendeshaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia kwa mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.

## Habari ambazo zitasaidia shule yako mpya kumpa mtoto wako kujifunza na usaidizi

Ni muhimu uipe shule yako mpya habari kuhusu mahitaji ya kujifunza na msaada wa mtoto wako. Ni muhimu kuiambia shule kuhusu mzio wowote unaojulikana au hali nyingine za matibabu zinazohusiana na mtoto wako.

Hii ni pamoja na lakini haizuiliwi kwa habari kwamba mtoto wako amegunduliwa kuwa na anaphylaxis, pumu, ugonjwa wa kisukari au kifafa.

Ikiwa mtoto wako amegunduliwa kuwa katika hatari ya kupata anaphylaxis tafadhali mpe shule mpya ya mtoto wako ASCIA Action Plan for Anaphylaxis ya sasa inayokamilishwa na kutiwa saini na daktari wa mtoto wako.

Pamoja na ASCIA Action Plan shule itahitaji autoinjector ya adrenaline kusaidia majibu ya dharura ya afya yaliyofafanuliwa katika mpango huo. Tafadhali kumbuka tarehe ya kumalizika muda wake kwenye autoinjector ya adrenaline iliyotolewa kwa shule na kutoa kifaa mbadala kabla ya wakati.

## Maelezo ya kukusaidia kukamilisha Semi la Nia

### Sehemu ya A

Tafadhali kamilisha maelezo ya kibinafsi ya mtoto wako na tia saini kwenye tamko katika **Sehemu ya A**.

### Sehemu ya B

**Sehemu ya B** huonyesha jina la shule yako iliyoteuliwa, kulingana na anwani ya nyumbani ya mtoto wako. Mtoto wako ana haki ya kupata nafasi katika shule za mtaa wake.

Ikiwa unatafuta uwekaji katika shule ya mtaa wako tu tafadhali tia saini kwenye **Sehemu ya B**, na rudisha fomu ile kwa tarehe inayotakiwa. Sasa umekamilisha fomu hiyo.

Ikiwa umeomba shule ya kuchagua kitaaluma, na unataka mtoto wako ahudhurie shule ya mtaa ikiwa hakufanikiwa, pia tia saini na weka tarehe kwenye **Sehemu ya B**.

## Sehemu ya C

Ikiwa unatafuta uwekaji mwingine tafadhali orodhesha hadi shule tatu kwa utaratibu wa upendeleo katika **Sehemu ya C**..

Unaweza kuomba uwekaji katika:

- shule maalum
- darasa la usaidizi (kwa kushauriana na mkuu wa shule yako ya msingi) ambaye atawasilisha ombi la kuomba aina ya darasa la usaidizi
- shule ya nje ya mtaa.

**Tafadhali kumbuka kuwa shule za kitaalamu, na paneli za uwekaji wa kuandikisha katika shule zisizo za mitaa zitakuwa na mahitaji ya ziada ya maombi.**

Ikiwa huna uhakika kama unahitaji kujaza fomu yoyote ya ziada, tafadhali wasiliana moja kwa moja na shule ambayo unavutiwa nayo.

**Kuna hatua ya ziada ikiwa unaomba kuwekwa katika shule ya nje ya mtaa.**

**Shule zina vigezo vya uwekaji wa uandikishaji wa nje wa mtaa ambapo mahitaji ya uandikishaji wa nje wa mtaa yanazidi idadi ya nafasi yaliyopo chini ya bafa ya kikimo cha uandikishaji.**

Ikiwa unatafuta nafasi katika shule ya nje ya mtaa, tafadhali toa sababu za kutafuta nafasi ya kusoma nje ya  mtaa, kwa mfano:

- ndugu au dada tayari wameandikishwa shuleni
- ukaribu na upatikanaji wa shule
- upatikanaji wa shule ya jinsia moja
- sababu za kimatibabu
- usalama na usimamizi wa mtoto wako kabla na baada ya shule
- upatikanaji wa masomo au mchanganyiko wa masomo shuleni
- mazingira ya huruma
- muundo na uandalizi wa shule
- mabadiliko ya hivi karibuni katika mipaka ya eneo la mwingilio.

Jopo la uandikishaji wa shule litazingatia tu habari katika fomu hii na nyaraka zingine muhimu unazozitoa.

Ikiwa mtoto wako hapewi nafasi katika shule yako ya Chaguo la 1, mtoto wako atazingatiwa kwa kuwekwa katika shule yako ya Chaguo la 2, basi katika shule ya Chaguo la 3, ikiwa inafaa.

Ikiwa hutafanikiwa kupata nafasi katika mojawapo ya chaguo zako, shule itakujulisha. Shule inaweza kuonyesha kuwa umewekwa kwenye orodha ya kungoja na utapewa nafasi ikiwa moja itapatikana.

Ikiwa mtoto wako anapewa nafasi katika moja ya upendeleo wako wa shule ulioorodheshwa, hutapokea ofa kutoka kwa shule nyingine yoyote ambayo iko chini kwa upendeleo.

Ikiwa hakuna nafasi inayopatikana katika shule yoyote uliyoomba, mtoto wako atapewa nafasi katika shule yake ya mtaa iliyoorodheshwa katika **Sehemu ya B**, kulingana na kukubaliwa kwa ombi lako la kujiandikisha na shule hiyo.

Ikiwa unahisi haujatendewa haki au kwamba matokeo hayana maana, unaweza kuwasilisha rufaa. Rufaa hiyo itolewe kwa maandishi kwa mkuu wa shule ya sekondari.

## Sehemu ya D

**Ilkiwa umeomba kwa shule ya kuchagua kitaaluma** tafadhali tia tiki kwenye sanduku katika **Sehemu ya D** ya fomu hii na jaza **Sehemu ya B, C** au **Sehemu ya E** ikiwa mtoto wako hafanikiwi kupata nafasi katika shule ya kuchagua.

## Sehemu ya E

**Ikiwa huhitaji nafasi katika shule ya serikali tafadhali jaza Sehemu ya E.**

Kukamilika kwa **Sehemu ya E** kunafunga hatua zote na shule za serikali za NSW kuhusiana na uwekaji wa mtoto wako katika Year 7.



Idara ya Elimu ya NSW

# Usemi wa Nia (Expression of Interest)

Uwekaji wa Year 7 katika shule ya Serikali ya NSW.

Placement in Year 7 in a NSW Government school.

**Tafadhali jaza fomu hii katika Kiingereza.**

SRN [ ][ ][ ][ ][ ][ ][ ][ ][ ]

Kwa matumizi ya ofisi tu (wazazi/walezi wasijaze.) (Office use only)

## A. Habari ya mwanafunzi (A. Student information)

**Jina la familia**
**Family name**

**Jina la kwanza la kupewa**
**First given name**

**Ma/jina ya kati (lingine)**
**Middle (other) name/s**

**Jinsia** ☐ Kiume ☐ Kike
**Gender** Male Female

**Tarehe ya kuzaliwa** __ __ / __ __ / __ __ __ __
**Date of birth** *Siku Mwezi Mwaka*

**Anwani ya makazi** *(es. 1 High Street, Sydney, NSW, 2000)* **(Residential address)**

**Jina la mzazi/mlezi**
**Name of parent/carer**

**Nambari ya simu** *(mkononi)*
**Phone number** *(mobile)*

**Nambari ya simu** *(nyumbani)*
**Phone number** *(home)*

**Nambari ya simu** *(kazi)*
**Phone number** *(work)*

**Anwani ya barua pepe**
**Email address**

**Shule ya msingi ya mwanafunzi ya sasa (Student's current primary school)**

**Tamko (Declaration)**

Ninasema kwamba maelezo yaliyotolewa katika Usemi huu wa Nia, kwa kadiri ya ufahamu wangu na imani yangu, ni sahihi na kamili. Ninatambua kwamba, iwapo taarifa katika ombi hili baadaye zitathibitishwa kuwa za uwongo au za kupotosha, uamuzi wowote unaotolewa kutokana na ombi hili unaweza kubatilishwa. Ninaelewa kuwa uandikishaji wowote unaofuata mchakato huu wa uwekaji utazingatiwa na kukubalika kwa *Ombi la Kujiandikisha katika Shule ya Serikali ya NSW (Application to Enrol in a NSW Government School)*.

**Saini ya mzazi/mlezi (Signature of parent/carer)**

**Andika jina (Print name)**

**Tarehe** __ __ / __ __ / __ __ __ __
**Date** *Siku Mwezi Mwaka*

## B. Uwekaji katika shule ya serikali ya mtaa wako (B. Placement at local government school)

**Shule ya mtaa wako (Your local school)**

Tafadhali tia saini kwenye sehemu hii ukitaka mtoto wako kuhudhuria shule hii.

**Saini ya mzazi/mlezi (Signature of parent/carer)**

**Tarehe** __ __ / __ __ / __ __ __ __
**Date** *Siku Mwezi Mwaka*

Ikiwa umetia saini hapo juu na unataka mtoto wako ahudhurie shule hii pekee, sasa umejaza fomu hii.

## C. Kuzingatia kupewa uwekaji katika shule zingine za serikali
## C. Consideration to be given to placement at other government schools

**Ikiwa unapendelea kuwa mtoto wako ahudhurie shule isiyo ya mtaa, unaweza kutoa hadi ya mapendeleo matatu. Unaweza kujumuisha:**

- **shule ya kitaalam ya serikali.** Tafadhali kumbuka kuwa unatiwa moyo kutafuta usaidizi kutoka mkuu wa shule ya msingi ikiwa unataka mtoto wako kuzingatiwa kwa nafasi katika shule ya kitaalam.
- shule yenye **madarasa ya msaada** kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ya kujifunza na usaidizi. Tafadhali kumbuka kuwa hii ni kupitia paneli ya uwekaji. **Unapaswa kutafuta msaada kutoka mkuu wa shule ya msingi ikiwa unataka mtoto wako kuzingatiwa kwa nafasi ya darasa la msaada.**
- shule nyingine ya serikali **isiyo ya mtaa**. Tafadhali eleza sababu zako za kutafuta nafasi katika uwekaji usio wa mtaa kwenye sehemu ya chini ya ukurasa huu (na kwenye ukurasa wa 7 ikihitajika).

Ningependa kutafuta nafasi ya mtoto wangu katika shule ifuatayo/zifuatazo ya/za serikali:

| | |
|---|---|
| **Shule ya Chaguo ya 1**<br>**Choice 1 school** | |
| **Shule ya Chaguo ya 2**<br>**Choice 2 school** | |
| **Shule ya Chaguo ya 3**<br>**Choice 3 school** | |

Naelewa kuwa ikiwa mtoto wangu hajafanikiwa kupata nafasi katika mojawapo ya shule zilizo hapo juu, atawekwa katika shule ya mtaa iliyoorodheshwa kwenye Sehemu ya B.

**Saini ya mzazi/mlezi (Signature of parent/carer)**

**Tarehe**
**Date** ☐☐ / ☐☐ / ☐☐☐☐

*Siku* *Mwezi* *Mwaka*

## Matumizi ya mkuu wa shule ya msingi pekee (Primary school principal use only)

Primary school principals may wish to include comments to assist secondary school principals make placement decisions. These comments should refer to the reasons given by parents and carers.

**Signature of primary school principal**

**Date** ☐☐ / ☐☐ / ☐☐☐☐

*day* *month* *year*

**Jaza maelezo yaliyo hapa chini ikiwa unaomba nafasi katika shule zisizo za karibu. Hukuna haja kukamilisha sehemu hii ikiwa unaomba shule ya kitaalam au darasa la usaidizi.** Ikihitajika, unaweza kuambatisha maelezo ya ziada ili kuunga mkono ombi lako la nafasi katika shule zisizo za karibu. Rejelea kurasa za 2 na 3 kwa habari zaidi.

| | |
|---|---|
| **Jina la shule ya Chaguo ya 1**<br>**Name of Choice 1 school** | |

Tafadhali eleza sababu zako za kutafuta nafasi katika shule hii (rejelea vigezo mahususi vya uandikishaji vya shule).

## C. (kuendelea) C. (continued)

**Jina la shule ya Chaguo ya 2**
**Name of Choice 2 school**

Tafadhali eleza sababu zako za kutafuta nafasi katika shule hii (rejelea vigezo mahususi vya uandikishaji vya shule).

**Jina la shule ya Chaguo ya 3**
**Name of Choice 3 school**

Tafadhali eleza sababu zako za kutafuta nafasi katika shule hii (rejelea vigezo mahususi vya uandikishaji vya shule).

## D. Shule ya kuchagua kitaaluma (D. Academically selective school)

☐ Nimetuma maombi ya kuwekwa katika shule iliyochaguliwa kitaaluma. Mtoto wangu atakuwa akishiriki katika mtihani wa Shule za Upili za Kuchagua.
I have submitted an application for placement in an academically selective school. My child will be sitting for the Selective High Schools test.

*Iwapo mtoto wako hatafaulu kupata nafasi katika shule hii/hizi, tafadhali jaza pia Sehemu ya B, Sehemu ya C au Sehemu ya E katika fomu hii.*

## E. Nafasi haihitajiki (E. Placement not required)

Nahakikisha kuwa mtoto wangu hataomba nafasi katika shule ya Serikali ya NSW mwakani. Nimesoma na kuelewa maelezo kuhusu uwasilishaji huu ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa taarifa za kibinafsi. Mtoto wangu atahudhuria shule ifuatayo. *

I confirm that my child will not be seeking placement at a NSW Government school next year. I have read and understood the information about this submission including the collection of personal information. My child will be attending the following school.*

**Saini ya mzazi/mlezi** **(Signature of parent/carer)**

**Tarehe**
**Date**

__ __ / __ __ / __ __ __ __
*Siku* *Mwezi* *Mwaka*

* Utoaji wa taarifa hii haihitajika lakini ungethaminiwa.

**Tamko la Ufaragha (Privacy Statement)**

Taarifa ya kibinafsi iliyotolewa kwenye fomu hii inayoitwa **Semi la Nia – Nafasi katika Mwaka wa 7** katika shule ya Serikali ya NSW hukusanyikwa kwa madhumuni ya kuratiba maombi yanayowezekana ya kuandikisha Year 7 katika shule za Serikali za NSW. Habari zozote zinazotolewa kwa NSW Department of Education (**the Department**) (Idara ya Elimu ya NSW) zitatumiwa, kufichuliwa na kuhifadhiwa kulingana na sheria za faragha za NSW privacy laws.

Taarifa fulani zinahitajika na **the Department** ili kutimiza wajibu wake wa matunzo na wajibu ya sheria na kazi nyingine chini ya sheria ya afya ya umma, elimu na ulinzi wa watoto na ili kukidhi mahitaji ya kukusanya na kuripoti data chini ya makubaliano ya ufadhili ya Jumuiya ya Madola na Majimbo. Hayo yanaweza kuhusisha makadirio na tathmini ya matokeo ya mwanafunzi.

Taarifa yanaweza kufichuliwa kwa mashirika ya serikali ya Jimbo la NSW na ya Jumuiya ya Madola na mashirika mengine kwa madhumuni ya hapa juu na kama ilivyoidhinishwa au kuhitajikwa na sheria.

Taarifa zitahifadhiwa kwenye hifadhidata ya kielektroniki yenye imara. Unaweza kupata au kusahihisha taarifa kwa kuwasiliana na shule ya mtoto wako. Ikiwa una suala au lalamiko juu ya taarifa iliyokusanyika au jinsi ilivyotumiwa au kufichuliwa, unapaswa kuwasiliana na shule.

Ikiwa unachagua kutotoa taarifa iliyoulizwa inaweza kuwa na athari mbaya kwa uandikishaji wa mtoto wako, ufadhili wa shule au kuridhi mahitaji ya kielimu ya mtoto wako.

Maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa taarifa wakati mtoto wako ameandikishwa katika shule ya serikali ya NSW na jinsi tunavyolinda faragha yako, yanapatikana kwenye tovuti ya Department au kutoka shuleni. Unaweza kupata nakala ya Notisi ya Mkusanyiko wa Faragha ya the Department kwa https://education.nsw.gov.au/content/dam/main-education/about-us/rights-and-accountability/media/documents/privacy/collection-notice.pdf

Kwa wanafunzi waliojiandikishwa kwa sasa katika shule za msingi za Serikali ya NSW, tafadhali rejesha fomu hii kwa shule ya msingi ya mtoto wako. Kwa wanafunzi ambao hawajajiandikishwa kwa sasa katika shule ya msingi ya Serikali ya NSW, tafadhali rejesha fomu hii kwa shule ya sekondari ya Serikali ya NSW ambayo unakusudia kumwandikisha mtoto wako. **Masemi yote ya Nia lazima yarejeshwe kabla au kwa tarehe ya kutarajia.**



Tunatambua nchi za nyumbani za watu wote wa asili na kutoa heshima yetu kwa Nchi.

**Say hello**

@NSWDepartmentofEducation

@NSWEducation

@NSWEducation

education.nsw.gov.au

© 2023 NSW Department of Education

GPO Box 33, Sydney NSW 2001 Australia

Phone: 1300 679 332

NSW GOVERNMENT